# Seriklai kuendelea kutangaza utalii wa Zanzibar

NA MWANAJUMA MMANGA

**SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imeeleza kuwa itaendelea kuchukua jitihada za kuitangaza Zanzibar kiutalii ili kufikia lengo la kuongeza idadi yao na kuchangia ukuaji wa uchumi.**

Hayo yamo katika hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi Makamu wa Pili wa Rais iliyowasilishwa na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, ambaye alieleza kuwa katika mwaka wa fedha 2024/2025 watalii 736,755 waliingia nchini ikilinganishwa na watalii 638,498 mwaka 2023/2024.

Alieleza kuwa idadi hiyo ni ongezeko la asilimia 15 ambapo pamoja na ongezeko hilo, bado serikali imeendelea kutangaza utalii ndani na nje ya nchi ili kupata watalii na waekezaji wapya kuja kuekeza katika sekta hiyo.

Alieleza kuwa serikali pia imeazimia kufungua milango zaidi ya kitalii kwa baadhi ya nchi ikiwemo India na China ambapo itaweza kutangaza utalii kwa kupitia filamu maalum ya kuitangaza Zanzibar .

Alisema filamu hiyo ilifunguliwa rasmi nchini India na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Husein Ali Mwinyi pamoja na kuandaa 'Presidential Tour' kwa lengo la kufungua soko la utalii nchini China.

Alisema serikali hivi sasa inaedneela kuwaalika watu maarufu dunaini kuitembelea Zanzibar ili kuitangaza na kuhamasisha wafuasi wao kuja Zanzibar ili kuutangaza utalii.

"Kwa mwaka huu tulibahatika kupata ugeni wa mufti Menk kutoka nchi Zimbabwe ambao pamoja na ujumbe wake alishiriki katika matukio mbali mbaoli yaliyosaidia kuitangaza nchi yetu kimataifa", alisema Hemed.

Aliongeza kusema kuwa serikali iliandaa maonesho ya kiutalii kwa uwekezaji huko Nyamanzi, wilaya ya Magharibi 'B' ili kuongeza idadi ya wageni wanaokuja Zanzibar kwa lengo la kutangaza utalii.

Alisema pamoja na hayo pia serikali inaendelea kuweka mazingira mazuri ya utalii ili kuwavutia wageni wanakuja Zanzibar ili kuweza kuwanufaika rasilimali zilizopo.

Aliongeza kuwa serikali ya mapinduzi ya zanzibar inakusudia kuifanya Zanzibar kuwa kitovu cha utalii wa kisasa usio na msimu kwa kuwavutia wawekezaji na wageni wengi kutoka mataifa yote ulimwenguni.



*MKUU wa wilaya ya Kondoa, Fatuma Nyangasa, akishiriki na maofisa wa vyombo vya ulinzi na usalama, mamlaka ya kudhibiti dawa za kulevya (DCEA) na wananchi operesheni maalum ya kutokomeza kilimo haramu cha bangi katika Hifadhi ya Milima ya Haubi, wilayani Kondoa, mkoani Dodoma. (PICHA NA ALEX SONA).*

# Muheza waanza maandalizi kupokea mwenge wa uhuru

NA STEVEN WILLIAM, MUHEZA

**MIRADI ya maendeleo yenye thamani ya mabilioni ya shilingi inatarajiwa kukaguliwa katika mbio za mwenge wa uhuru mwaka 2025 wilayani Muheza mkoani Tanga.**

Akizungumza katika kikao cha mapokezi ya mwenge wilayani Muhezai mwaka huu, Mkuu wa wilaya, Zainab Abdallah, alisema mwenge wa uhuru unatarajiwa kupokelewa wilayani humo Juni 12 ukitokea wilaya ya Korogwe na utakabidhiwa Wilaya ya Pangani Juni 13.

Aidha, aliwaagiza viongozi mbalimbali wa walaya kufanya hamasa katika maeneo yao ili wananchi wajitokeze kwa wingi katika mapokezi ya mwenge.

Aliwaomba wananchi kujitokeza kwa wingi katika mapokezi ambako mwenge huo utakapopita katika miradi ya maendeleo.

Alisema ujumbe wa mwenge wa uhuru wa mwaka huu unaongozwa na kaulimbiu isemayo "Jitokeze kushiriki uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 kwa amani na utulivu".

# Wakulima wahimizwa kulima kibiashara

NA SALAMA MOHAMMED, WKUMM

**MKURUGENZI** Mipango, Sera na Utafiti wa Wizara ya Kilimo Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Makame Kitwana Makame, amesema ipo haja kwa wakulima kutumia uwezo wao kuzalisha mazao kibiashara ili kujiendesha kupitia kilimo.

Kitwana aliyasema hayo ofisini kwake Maruhubi Mjini Unguja katika mahojiano ya kipindi cha Mazungumzo ya Asubuhi yaliyokua yakiangazia uchambuzi wa bajeti ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, maliasili na misitu iliyopitishwa na Baraza la wawakilishi wiki iliyopita.

Aidha alisema mkulima yeyote kikawaida anatakiwa kuondokana na mawazo ya kulima kwa chakula peke yake na badala ya kufiikiria kulima kibiashara ili aweze kupata faida kutokana na kilimo chake.

Aliongeza kuwa kufanya hivyo kiutawasaidia kupata kipato kitakachokishi mahitaji yake na ziada ambayo atauza na kuifanya nchi kuwa na chakula cha kutosha pamoja na mapato yanayotokana na kilimo.

"Hivi sasa nchi yetu ina mahitaji mengi hasa katika upatikanaji wa chakula pamoja na uwepo wa mahitaji mengi ya bidhaa maalum katika masoko ya kimataifa hivyo ni vyema mkulima anayelima kwa ajili ya chakula angalie mtazamo wake na badala yake alime kibiashara kwa ajili ya kuongeza kipato katika kilimo chao", alieleza Kitwana.

Kitwana pia alieleza kuwa mfumo wa sasa kwa Mabwana na Mabibi shamba kwenda moja kwa moja kwa mkulima umekuwa na faida licha ya kukabiliwa na changamoto inayotokana na idadi kubwa ya wakulima.

Alisema kutokana na wingi wao imekuwa vigumu kuwafikia wakulima kwa wakati ikilinganisha na idadi ndogo ya mabwana shamba na kuongeza haja ya kutumika kwa teknolojia ili kupunguza masafa wanayotumia na kurahisisha ufikiwaji wao.

# Washauriwa kuvuna maji ya mvua

NA BOAZ JULIUS, MOROGORO

**BODI ya Maji Bonde la Wami Ruvu imewashauri Watanzamia kuweka miundombinu ya kuvuna maji ya mvua zinazoendelea kunyesha ili waondokane na tatizo la maji.**

Wito huo ulitolewa na Mkurugenzi wa Bodi hiyo, Mhandisi Elibariki Mmassy, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari mjini Morogoro ambapo alisema maji ya mvua hayana gharama kubwa kuyavuna tofauti na kuchimba kisima.

"Ili mtu aweze kuchimba kisima anahitaji zaidi ya shilingi milioni 10 jambo ambalo baadhi ya watu hawawezi kumdu gharama hizo, lakini kwa upande wa miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua ni shilingi milioni tatu, hivyo ni rahisi,"alisema Mmassy.

Alisema mtu akivuna maji ya mvua na kuyahifadhi vizuri, anaweza kuyatumua mwaka mzima hadi msimu mwingine wa mvua ambapo aliwataka waandishi wa habari kutumia kalamu zao kuwaelimisha wananchi juu ya suala hilo.

Alisema bodi hiyo itahakisha inatoaushirikiano kwa mtu yeyote atakayehitaji msaada wa kuweka miundombinu ya kuvuna maji ya mvua nyumbani kwake ambapo pia aliwaomba wote wanaohitaji kuchimba visima kuhakikisha wanafuata utaratibu ili kukwepa mkono wa sheria.

Aidha aliwataka wakulima wenye vibali wanaofanya shughuli zao pembezoni mwa mito au vyanzo vya maji kuacha kutupa vifungashio vya viuatilifu kwenye mito kwani vina simu, hivyo vinaweza kunahatarisha usalama wa watumiaji.

Mkuu wa kidakio cha Ruvu,Mhandisi Paschal Joseph, alisema hali ya upatikanaji maji mto Ruvu ni nzuri ambapo aliwaomba wananchi kuendelea kutunza vyanzo vya maji kwa kujiepusha na shughuli za kibinadamu.

Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi wa Habari Mkoa wa Morogoro (MOROPC), Nickson Mkilanya, alisema waandishi wa habari wa mkoa huo wataendelea kushirikiana ipasavyo na uongonzi wa Bodi hiyo ili kuongeza ufanisi kwa masilahi na taifa.